

Maswali kuhusu chanjo za COVID-19



Je, athari za chanjo ya COVID-19 ni zipi?

Ni kawaida kwa watu kuwa na dalili nyepesi au za wastani au athari baada ya kupata chanjo. Dalili nyepesi au wastani ni pamoja na vitu kama homa au wekundu karibu na mahali walipodungwa sindano ya chanjo.

Kwa kawaida hakuna sababu ya kuwa na wasiwasi ikiwa unapata dalili nyepesi hadi wastani siku chache baada ya kupata chanjo. Hii inamaanisha mwili wako umeanza kufanya kazi ili kuunda mwitikio wa kinga na unajifunza kupambana na ugonjwa huo.



Je, chanjo ya COVID-19 itagharimu pesa ngapi?

Dozi za chanjo ya COVID-19 zilizonunuliwa na fedha za walipa kodi wa Marekani zitatolewa kwa kila mtu bila malipo. Ikiwa una bima, watoaji wa chanjo wanaweza kutoza bima yako ada ya maalum ya kutoa, au kutekeleza, chanjo. Lakini hakuna mtu anayepaswa kunyimwa chanjo ikiwa huna uwezo wa kulipa.

Je, lazima niwe raia wa Marekani, mkazi wa Marekani, au ninahitaji kuwa na visa ili kupata chanjo?

La. Hali yako ya uhamiaji haitakuzuia kupata chanjo. Maelezo yako ya kibinagsi ni ya siri na yanalindwa na sheria. Ikiwa uko katika moja ya vikundi vyta kitengo cha hatari kupata chanjo hivi sasa, wasiliana na mwajiri wako au idara ya afya ya eneo lako kwa maelezo zaidi. Huenda ukahitaji kuonyesha uthibitisho kuwa unafanya kazi huko sasa hivi, kama beji yako ya kazi.





Je, ninahitaji kitambulisho kupata chanjo?

Watoaji wengine wa chanjo watakuomba tu uonyeshe uthibitisho wa barua pepe uliyopata baada ya kusajili miadi yako ya chanjo, lakini watoa huduma wengine wanaweza kukuomba uonyeshe kitambulisho chenye picha wakati wa miadi yako.

Tunatumia tu maelezo yako ya kibinafsi kwa vitu 2:

- 1 Kuhakikisha kuwa umefikisha umri wa kupata chanjo.
- 2 Kuhakikisha tunachanja mtu anayefaa kuchanjwa. Lazima tuhakikishe jina la mtu anayepata chanjo linalingana na jina kwenye miadi. Utahitaji dozi ya pili ya chanjo wiki chache baada ya ile ya kwanza. Hati zote zinapaswa kufanana ili tuweze kuhakikisha kuwa hakuna shida yoyote unapokuja kupata dozi yako ya 2.



Hatufichui maelezo yako kwa watekelezaji sheria au maafisa wa uhamiaji.

Unaweza kutumia aina tofauti za kitambulisho chenye picha kwa watoaji wengi wa chanjo. Watahitaji tu kitambulisho kilicho na picha yako, jina, na tarehe ya kuzaliwa. Unaweza kuhitaji kuleta aina tofauti ya ithibati kwamba unaishi katika kaunti, kama bili ya gesi au huduma, ikiwa kitambulisho chako hakina anwani yako.

Wasiliana na idara yako ya afya au mtoaji wa chanjo ikiwa una maswali yoyote.

Ikiwa unapata chanjo na mwajiri wako, huenda ukalazimika kuonyesha uthibitisho unafanya kazi hapo sasa, kama beji yako ya kazi.



Kwa maelezo zaidi kuhusu COVID-19, chanjo za COVID-19, au ni lini na wapi unaweza kupata chanjo, tembelea <https://coronavirus.utah.gov/>.

Unaweza kujiandikisha kwenye tovuti kufahamishwa wakati taarifa mpya ya chanjo inapatikana.

Ikiwa una maswali kuhusu COVID-19 au chanjo, piga simu kwa nambari ya simu ya dharura ya COVID-19 katika **385-273-7878**. Simu hiyo ina watalamu makinifu wa afya ambao wanaweza kukusaidia kujibu maswali yako na kupata rasilimali karibu nawe.

Inapatikana 24/7 katika lugha zaidi ya 100.